

# 2021

## TCCIA INVESTMENT PLC

MKUTANO MKUU WA MWAKA
WA 16 WA WANAHISA 20/11/2021




# TAARIFA YA KAMPUNI

Kwenye Mkutano Mkuu wa 16 wa Wanahisa

# TAARIFA YA KUITISHA MKUTANO NA AKIDI

Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na kifungu Namba 33 cha Kanuni za Kampuni kinachohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu Maalum wa Wanahisa.

Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa kifungu Na. 38 cha Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasiopungua 10 wanaomiliki hisa Zaidi ya asilimia 50.



## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA

UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 20 NOVEMBA, 2021.
Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na sita wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 20 Novemba, 2021 kwa njia ya mtandao.

# KUPOKEA AJENDA

Wanahisa mnaombwa kupokea Ajenda kama ilivyowasilishwa.



Dondoo Na. 16/1/2021

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA SITA UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 20 NOVEMBA 2021.

Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na sita wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 20 Novemba, 2021 kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3:00) asubuhi. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.

**Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita ni:**

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita;
2. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita;
3. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano;
4. Yatokanayo na Mkutano wa Kumi na Tano;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2020;
6. Kupokea na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2020;
7. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 31 Desemba, 2021;
8. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi;
9. Kupokea, na kuridhia pendekezo la mabadiliko kwenye daftari la Wanahisa;
10. Kupokea, kujadili na kuamua mapendekezo kutoka kwa Wanahisa;
11. Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi;
12. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Sita.

**Maelezo:**

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 10 yatumwe na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 7 Novemba, 2021;
2. Taarifa ya Mwaka 2020 na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https://www.tcciainvest.co.tz) na kuanzia tarehe 8 Novemba, 2021;
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa kuteua Mwakilishi atakayehudhuria Mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https:// www.tcciainvest.co.tz). Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe info@tcciainvest.co.tz au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na. 0757-138048 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 17 Novemba, 2021.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

**Peter W. Kifunguomali**
Katibu
Tarehe_______

Dondoo Na. 16/2/2021

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI, TAREHE 22 AGOSTI, 2020 KWA NJIA YA MTANDAO.

## 15.1 WALIOHUDHURIA

Bw. Fortunatus Magambo - Mwenyekiti

Bw. Peter W. Kifunguomali - Katibu

Orodha ya Wajumbe pamoja na Wawakilishi wa Wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano uliofanyika siku ya Jumamosi tarehe 22 Agosti, 2020 imeambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1.

## 15.2 KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO

Mwenyekiti alifungua Mkutano kwa kuwakaribisha Wanahisa, Wajumbe wa Bodi, Wageni Waalikwa na Wafanyakazi wa Kampuni kwenye Mkutano Mkuu wa 15 wa Mwaka. Baada ya Kutolewa taarifa kwamba Akidi ilikuwa imetimia kulingana na Kifungu Namba 38 cha Kanuni za Kampuni, Mwenyekiti alifungua Mkutano saa 3:00 Asubuhi.

## 15.3 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO.

Hakukuwa na Mabadiliko yoyote hivyo Wajumbe walipitisha Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano kama zilivyosomwa na Katibu wa Bodi.

## 15.4 MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI.

Wanahisa waliombwa kuongeza katika kifungu cha 47 na 86 cha Kanuni za Kampuni ili kuonyesha kuwa Mikutano Mikuu inaweza kufanyika kwa njia ya kukutana ana kwa ana au kwa njia ya mtandao na idadi ya Wanahisa wasiopungua 10 wenye hisa zaidi ya asilimia 50.

15.4.1 Iliazimiwa kwamba kifungu cha 47 kisomeke kuwa "Kampuni itafanya Mkutano Mkuu wa kila mwaka ama kwa Wanahisa kukutana ana kwa ana au kwa njia ya mtandao. Pia iliazimiwa kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 86 kuwa Mkutano Mkuu utahudhuriwa na Wanahisa wasiopungua 10 wenye hisa zaidi ya asilimia 50.

## 15.5 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE.

Wajumbe walithibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne na zikasainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

## 15.6 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO ULIOFANYIKA TAREHE 22 AGOSTI, 2020.

Taarifa ilitolewa kuhusu utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na Wajumbe wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano uliofanyika tarehe 22 Agosti, 2020 na kukubaliwa na Wanahisa.

## 15.7 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019.

**Taarifa ya Wakurugenzi iliwasilishwa na Prof. Lucian Msambichaka kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.**

**15.7.1** Majadiliano kutoka kwa Wanahisa ni kama ifuatavyo;

**15.7.1.1** Waliipongeza Bodi ya Wakurugenzi kwa Taarifa nzuri;

**15.7.1.2** Ni vema Bodi iendelee kuangalia namna ya kuongeza mapato ya Kampuni na kuepuka matumizi yasiyo ya lazima;

**15.7.1.3** Kuangalia fursa mbalimbali katika uwekezaji katika sekta ya viwanda;

**15.7.2** Maswali na mapendekezo yalitolewa ufafanuzi kama ifuatavyo;

**15.7.2.1** Mwenyekiti aliwajulisha wajumbe kuwa, Kampuni imeshachukua hatua ya kuwekeza katika Amana za Serikali na sasa inafanya mpango wa kuwekeza kwenye maduka ya kuuza na kununua fedha za kigeni (Bureau De Change);

**15.7.2.2** Bodi imeshachukua hatua stahiki ya kupunguza matumizi na kupunguza idadi ya wajumbe wa Bodi kutoka 11 na kufikia 7.

## 15.8 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA MAHESABU YA KAMPUNI YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019.

**15.8.1** Taarifa ya Mahesabu iliwasilishwa na haikukinzana na taarifa nyingine. Kulingana na Taarifa ya mahesabu, shughuli za Kampuni zitaendelea bila kuathirika na chochote. Mkaguzi wa mahesabu aliwajulisha wajumbe kuwa, Kwa mwaka wa fedha wa 2019, Kampuni Ilipata Hati safi. Iliazimiwa kwamba Taarifa ya mahesabu ya kampuni yaliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2019 yamepitishwa kama ilivyowasilishwa.

**15.8.2 AZIMIO KUHUSU MALIPO YA GAWIO**

Taarifa ilitolewa kuwa Azimio hili limetekelezwa kwa kuwalipa Wanahisa ambao taarifa zao katika Daftari la Wanahisa zilikuwa zimerekebishwa. Kila Mwanahisa alilipwa shilingi 6 kwa kila hisa moja.

### 15.9 KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA BODI KUHUSU MALIPO YA GAWIO KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019.

Bodi ilipendekeza kuwa malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio. Kwa Wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

**15.9.1** Mkutano Mkuu uliazimia na kuridhia gawio la shilingi za Kitanzania (6) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi.

### 15.10 UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2020

Bodi ilipendekeza kuwa, CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2020. Ada ya Ukaguzi iliyopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 19 milioni kabla ya VAT. Ilielezwa kuwa ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

**15.10.1** Iliazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2020. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 19 milioni kabla ya VAT kama gharama za malipo ya ukaguzi wa mahesabu ya Kampuni.

### 15.11 PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Mkutano Mkuu uliarifiwa kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2019, Menejimenti ilipendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000), kwa kuwa kiasi hiki kimezingatia mazingira ya sasa na pia Wakurugenzi walikuwa wakilipwa kiasi cha shilingi milioni nne kwa kipindi cha miaka minne.

**15.11.1** Iliazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi.

**Katibu:**_____________ **Mwenyekiti**___________________

Tarehe:____________

Dondoo Na. 16/2/2021

## KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 22 AGOSTI 2020

**WASILISHO**

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika tarehe 22 Agosti, 2020 kama kumbukumbu sahihi ya mkutano mkuu wa 15 wa Mwaka kwa kuazimia kama ifuatavyo:-

### “Azimio la 1/2021

Imeazimiwa kuwa Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa kumi na Tano ulifanyika tarehe 22 Agosti 2020 ni kumbukumbu sahihi”

## YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO ULIOPITA

| Kumb | Maelezo mafupi | Azimio | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| **15.4.1** | Mabadiliko ya vifungu vya MEMART | Kuongeza kifungu cha 47 na 86 cha Kanuni za Kampuni ili kuonyesha kuwa Mikutano Mikuu inaweza kufanyika kwa njia ya kukutana ana kwa ana au kwa njia ya mtandao na idadi ya Wanahisa wasiopungua 10 wenye hisa zaidi ya asilimia 50. | Agizo hili limetekelezwa na kusajiliwa BRELA |
| **15.4.1** | Malipo ya Gawio | Gawio lilipwe Shilingi sita (6) kwa kila hisa moja. | Limetekelezwa kwa wale ambao taarifa zao zimekamilika. |
| **15.10.1** | Kuteua Mkaguzi wa Mahesabu | Mkutano Mkuu uliidhinisha CROWE Tanzania kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2020 | Limetekelezwa. |
| **15.11.1** | Malipo ya Wakurugenzi | Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi 4,800,000 kwa kila mjumbe kwa mwaka 2019. | Limetekelezwa. |



Dondoo Na. 16/4/2021

## KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2020.

Taarifa ya Fedha ya mwaka iliyokaguliwa iko katika Taarifa ya Mwaka.

# TAARIFA YA MWENYEKITI

*"Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wanahisa wetu wote, wateja na washirika wetu katika biashara kwa kuendelea kutuamini na kufanya kazi pamoja, Bodi ya Wakurugenzi kwa mwongozo wao mzuri, wafanyakazi wote kwa mchango wao katika kufanya kazi kwa bidii licha ya changamoto mbalimbali zinazojitokeza. Tutaendelea kufanya kazi kwa bidii kukabiliana na changamoto zinazojitokeza ili kukuza ongezeko la thamani katika biashara za Kampuni."*

*Fortunatus M. Magambo*



Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ninayo furaha kuwasilisha taarifa ya utendaji kwa mwaka 2020. Pamoja na changamoto ya ugonjwa wa Corona (Uviko – 19), bado Kampuni imeendelea kufanya vizuri. Kufikia mwishoni mwa Disemba, 2020 mapato yaliongezeka kwa asilimia 40 ukilinganisha na mwaka 2019. Hata hivyo faida baada ya kodi ilipungua kwa asilimia 215 ukilinganisha na mwaka uliopita. Hii ni kutokana na mabadiliko ya mbinu za uwekezaji kutoka uwekezaji kweye hisa za makampuni kwenda kwenye hati fungani za serikali.

**BIASHARA ENDELEVU**

Kampuni ina malengo ya muda mrefu katika kutimiza maono yake, dhima na maadili ya msingi yanayojumuisha nyanja tatu ambazo ni: Ongezeko la thamani kwa Wanahisa, ubora wa uwekezaji, na ubora katika utendaji. Ili Kampuni kuendelea na shughuli zake za kibiashara tunaamini kuwa, kufanya kazi pamoja kwa kushirikiana na wadau wetu wakuu kunaweza kuleta ufanisi zaidi na mazingira salama ya kiutendaji. Uimara wa Kampuni ni nguzo muhimu katika utendaji na kutokana na malengo mapya tuliyonayo tutaweza kuchukua hatua madhubuti.

Licha ya dalili zilizojitokeza za kupungua kwa mauzo katika Soko la Hisa, kushuka kwa thamani ya hisa, kutofanya vizuri kwa baadhi ya kampuni ambapo TICL imewekeza, bado Kampuni imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kukuza mtaji na kuongeza faida. Tunapotazamia hali ya Soko la Hisa kwa siku zijazo, bado inaonekana kuwa Soko litaendelea kutokuwa na uhakika wa kufanya vizuri kulingana na maambukizi ya Uviko – 19 kusambaa sehemu mbali mbali duniani. Licha ya changamoto hizi za mpito, tutaendelea kuwekeza katika vyanzo mbali mbali vya mapato, kuwaelimisha wafanyakazi wa Kampuni katika kukabiliana na changamoto hizi ili kuwa na biashara endelevu kwa siku zijazo.

Kuwa na uwezo wa kutengeneza faida hata katika mazingira magumu ni moja ya malengo mapya ya kifedha ambayo yameainishwa katika Mpango Mkakati wa Kampuni kwa mwaka 2020 - 2022. Kampuni ina mpango wa kuwekeza katika vyanzo mbalimbali vya mapato na kuacha kutegemea chanzo kimoja ili kuimarisha mapato. Tunalenga kuongeza faida kwa asilimia 22 kwa mwaka.

## GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Disemba 31, 2020, Bodi inapendekeza malipo ya gawio yawe Shilingi 6 kwa hisa moja au shilingi 475.19 millioni kama ilivyokuwa mwaka 2019. Malipo ya gawio yaliyopendekezwa yanategemea kuidhinishwa na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu huu wa 16.

## MATARAJIO YA BAADAYE

Kwa mwaka 2021, Bodi itajikita katika utekelezaji wa mipango iliyowekwa ya kukuza vyanzo vya mapato na kukuza ufanisi wa kazi. Kutokana na mafunzo mbali mbali tuliyopitia, tunatarajia kuja na mipango madhubuti ili kuhakikisha kuwa tunakuza vyanzo vya mapato ambavyo vitasaidia kufikia malengo na matarajio yetu kwa kuzingatia fursa mpya zitakazojitokeza.

## SHUKRANI

Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wanahisa wetu wote, wateja na washirika wetu katika biashara kwa kuendelea kutuamini na kufanya kazi pamoja, Bodi ya Wakurugenzi kwa mwongozo wao mzuri, wafanyakazi wote kwa mchango wao katika kufanya kazi kwa bidii licha ya changamoto mbalimbali zinazojitokeza. Tutaendelea kufanya kazi kwa bidii kukabiliana na changamoto zinazojitokeza ili kukuza ongezeko la thamani katika biashara za Kampuni.

Napenda pia kuwashukuru Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na mamlaka zingine kwa msaada na mwongozo wao mzuri.

Nawashukuru pia Bodi ya Wakurugenzi kwa juhudi zao katika kuiwezesha Kampuni kuendelea kufanya vizuri na utekelezaji wa Mpango Mkakatati wa mwaka tuliojiwekea.

Kwa niaba ya Bodi, napenda kuishukuru Kamati ya Usimamizi kwa kusimamia vyema na kuweza kutekeleza vipaumbele vilivyowekwa na Bodi. Ninawashukuru pia wafanyakazi wetu wote wa Kampuni kwa kufanya kazi kwa bidii na kujitoa ili kuongeza mapato na ongezeko la thamani kwa Wanahisa.

Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zetu kwa Wanahisa kwa kuendelea kuwa pamoja nasi na kuiamini Kampuni. Tunapoendelea na safari hii, nina imani kuwa kwa pamoja tunaweza kufanya vizuri zaidi. Kwa Wanahisa na wadau wetu wote, tunasisitiza kuendelea kujitoa na kuongeza juhudi katika kazi.

Ahsanteni sana.

**Fortunatus M. Magambo**
Mwenyekiti wa Bodi
Tarehe:**12/05/2021**

# TAARIFA YA MTENDAJI MKUU



*Tuna imani ya kukamilisha malengo tuliyojiwekea kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa 2021 na kupata faida. Japokuwa Soko halifanyi vizuri, bado Kampuni imeendelea kufanya vizuri, na kutuweka kwenye nafasi nzuri katika ushindani wa uwekezaji. Kwa mwaka huu wa 2021 tunategemea pia kupata faida.*

*Peter William Kifunguamali*

Kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2020, tumepiga hatua mbalimbali katika kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitatu wa Kampuni. Mapato yameongezeka kwa asilimia 40 wakati gharama za uendeshaji zikipungua kwa asilimia 0.05. Tumefanikiwa kuwalipa wanahisa gawio kama ilivyokuwa mwaka uliopita. Mwaka 2020, umekuwa ni mwaka wa kwanza katika kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka mitatu ambao umejikita katika maeneo muhimu manne ambayo ni; Ufanisi wa huduma, kuongeza faida, kurahisisha mzunguko wa fedha na kuongeza mapato. Bodi na Wafanyakazi wameendelea kuimarisha ongezeko la thamani kwa wanahisa wetu na ubora katika uwekezaji. Tunaendelea kukuza ongezeko la thamani la muda mrefu kwa wanahisa na kuimarisha uwekezaji kulingana na ushindani. Tumefanya maamuzi kadhaa muhimu katika kutekeleza hili ikiwa ni pamoja na kupunguza uwekezaji katika hisa na kuwekeza zaidi katika amana za serikali ambazo zimewezesha mapato ya Kampuni kuongezeka kwa Shilingi 720 millioni kwa mwaka 2020.

## TAARIFA YA KIUTENDAJI

Kampuni imeendelea kufanya vizuri. Mapato pamoja na uwekezaji vimeongezeka kwa mwaka 2020 ukilinganisha na taarifa ya 2019 kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

| Maelezo | Maelezo | 2020 | 2019 | Makisio |
|---|---|---|---|---|
| Mapato | Shilingi'000 | 2,507,571 | 1,901,959 | kutokana na ongezeko kwenye hatifungani |
| Gharama za Uendeshaji wa Kampuni | Shilingi'000 | 1,060,243 | 1,060,795 | Dumisha |
| Faida baada ya Kukata Kodi | Shilingi'000 | (475,136) | 409,714 | Kulingana na Mabadiliko ya Kanuni ya Kimataifa ya Uaandaji wa Taarifa za Mahesabu (IFRs 9) baada ya kuuza hisa (Ni hasara ya kimahesabu vitabuni tu na sio katika mzunguko wa kifedha |
| Mali za wanahisa | Shilingi'000 | 26,570,955 | 27,096,381 | Imechangiwa kwa kiasi kikubwa na hasara iliyopatikana |

| Maelezo | Maelezo | 2020 | 2019 | Makisio |
|---|---|---|---|---|
| Thamani ya kila Hisa (mali ukiondoa madeni) | Shilingi'000 | 69 | 70 | Dumisha |
| Mapato kwa kila Hisa | Shilingi | (6.51) | 5.62 | Kulingana na Mabadiliko ya Kanuni ya Kimataifa ya Uaandaji wa Taarifa za Mahesabu (IFRs 9) baada ya kuuza hisa (Ni hasara ya kimahesabu vitabuni tu na sio katika mzunguko wa kifedha |
| Gawio kwa kila Hisa | Shilingi | 6 | 6 | Dumisha |

## UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2020

Kwa mwaka 2020, kazi kubwa iliyofanywa na Kampuni ni kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Kampuni iliwekeza jumla ya Shilingi 3.9 bilioni kwenye Amana za Serikali (Government Bonds). Kampuni iliuza hisa inayomiliki katika makampuni mengine yenye thamani ya Shilingi 3.6 bilioni kama sehemu ya mkakati wake wa kuwekeza kwenye vyanzo vingine vya mapato. Kwa mwaka 2020, ilibadili mkakati wa uwekezaji kuacha kutegemea chanzo kimoja cha mapato ila kwa kuzingatia Kanuni za Kampuni na Sera ya Uwekezaji. Maeneo ambayo Kampuni imewekeza ni Pamoja na Amana za serikali, Amana za Makampuni, Amana za mabenki, Hisa na uwekezaji kwenye mali zisizohamishika. Maeneo ambao Kampuni iliwekeza kufikia Desemba 31, 2020 kwa muhtasari ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

| Aina ya Uwekezaji | 31/12/2020 (Shilingi'000') | % | 31/12/2019 (Shilingi'000') | % | 31/12/2019 (Shilingi'000') | % ya mabadiliko |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Hisa | 14,848,114 | 51.52 | 19,364,888 | 65.58 | (4,516,774) | (23) |
| Amana za Serikali | 13,578,175 | 47.12 | 9,678,019 | 32.77 | 3,900,156 | 40 |
| Amana za Benki | 155,000 | 0.54 | 210,415 | 0.71 | (55,415) | (26) |
| Amana za Kampuni | 10,000 | 0.03 | 30,336 | 0.10 | (20,336) | (67) |
| Mali zisizohamishika | 221,347 | 0.77 | 239,820 | 0.81 | (18,473) | (8) |
| Maeneo mengine | 5,500 | 0.02 | 5,500 | 0.02 | - | - |
| **Jumla ya Uwekezaji** | **28,818,136** | | **29,528,978** | | **(710,842)** | **(2)** |

Tuna imani ya kukamilisha malengo tuliyojiwekea kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa 2021 na kupata faida. Japokuwa Soko halifanyi vizuri, bado Kampuni imeendelea kufanya vizuri, na kutuweka kwenye nafasi nzuri katika ushindani wa uwekezaji. Kwa mwaka huu wa 2021 tunategemea pia kupata faida.

## MPANGO WA KAMPUNI KWA MWAKA 2020-2022

Katika kufikia mpango mkakati mwaka 2022 katika kuongeza mapato, Kampuni inategemea kufungua dirisha la Uuzaji wa Amana za makampuni na kuwekeza kwa niaba ya makampuni mengine.
Wakati huu Kampuni ikiendelea kukua, pia tutaendelea kulinda utawala bora na usimamizi wa athari zinazoweza kujitokeza. Mwisho, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanahisa wote, Bodi ya Wakurugenzi, kamati ya usimamizi, mabenki, Wakaguzi wa mahesabu na Wawekezaji kwa kujitoa kwao bila kuchoka kusaidia Kampuni yetu.

***Ahsanteni Sana***



**Peter William Kifunguomali**
Afisa Mtendaji
Tarehe:**12/05/2021**

# TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2020 UTANGULIZI

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Wakurugenzi pamoja na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2020. Taarifa hii inatoa picha kamili ya hali halisi ya Kampuni.

## UANZISHWAJI WA KAMPUNI

Kampuni ilianzishwa Novemba, 1999 na kuanza shughuli za biashara Januari, 2005. Kampuni inafanya biashara kwa njia ya Uwekezaji wa pamoja ambapo wanachama wa TCCIA waliweza kukusanya mtaji kwa lengo la kununua hisa kupitia agizo la Serikali la kutaka kuibinafsisha Benki ya NMB.
Kufikia Disemba 31, 2020, jumla ya wanahisa walikuwa 3,426 ambapo PSSSF ni shirika pekee ambalo linamiliki asilimia 38.5 ya hisa zote za Kampuni. Wanahisa waliobaki ni watu binafsi na baadhi ya makampuni madogo na ya kati.

## BIASHARA YA KAMPUNI

Kulingana na Katiba ya Kampuni (MEMARTS), biashara kuu ya Kampuni ni uwekezaji katika viwanda, taasisi za fedha, huduma za mawasiliano, kilimo, madini, ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo na huduma za kijamii.

**MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI:-**

**DHIMA YA KAMPUNI**
Kutengeneza ongezeko la thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wa Kampuni kwa kutoa faida nzuri zaidi inayotokana na uwekezaji bora na salama.

**MAONO YA KAMPUNI**
Kuwa kituo kikuu cha usimamizi wa uwekezaji Tanzania.

**KAULI MBIU**
Kwa pamoja tunaweza.

**MAADILI KATIKA KAZI:**
Uwajibikaji, Kujitoa, Kufanya kazi kwa pamoja, Uaminifu na uvumbuzi.

## DHUMUNI NA MPANGO MKAKATI WA KAMPUNI

Ongezeko la Thamani: Kuiwezesha Kampuni kufikia lengo la wanahisa la kuanzishwa kwa hii Kampuni. Lengo kuu ni kuongeza thamani ya Hisa na kukuza mtaji wa Kampuni. Kampuni pia inalenga kuanzisha Kampuni tanzu ili kugawanya mtaji wake katika maeneo mengine ya biashara.
Uwekezaji Bora: Kampuni ina lengo la kuimarisha thamani ya Kampuni kwa kuimarisha rasilimali za Kampuni na kuongeza kipato katika uwekezaji. Kampuni ina mpango wa kukuza kipato kupitia uwekezaji kwa asilimia ishirini na mbili (22%) kwa mwaka.
Utendaji Bora: Kampuni ina mpango wa kuimarisha utendaji kupitia wafanyakazi waliopo na teknolojia ili kukuza ufanisi, kuhudumia wanahisa, kukidhi matakwa ya mamlaka zinazoisimamia, kuimarisha utamaduni wa ushirikiano, kuimarisha maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha utendaji na uwajibikaji wa wafanyakazi. Kampuni ina mpango wa kufanikisha mipango yake kwa asilimia tisini na tano (95%).

## BIASHARA ENDELEVU

Katika majadiliano ya Bodi katika kuimarisha ukuaji wa Kampuni, haukuzingatia kushuka na kupanda kwa thamani ya fedha. Bodi ilizingatia kulinda na kuhakikisha Kampuni inaendeleza utendaji wake, mabadiliko ya tabia nchi na rasilimali zinazohitajika ili Kampuni iendelee kufanikiwa kwa miaka ijayo. Lakini pia tunaamini katika kuimarisha mazingira ya utendaji katika kuepuka kuwekeza kwenye miradi ambayo itaharibu sifa nzuri ya Kampuni hata kama utakuwa na faida kubwa; kuhimiza wafanyakazi na wadau wa Kampuni kujiendeleza, kujizoeza na kutumia teknolojia, kutumia mtandao, kuongeza upeo wa wafanyakazi wa TICL katika utendaji na kuwahimiza wadau wa Kampuni kuhusu kuondoa madhara ya kimfumo kupitia teknolojia.

## WAKURUGENZI WA KAMPUNI

Kwa mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2020, Wakurugenzi walikuwa:-

| JINA | NAFASI | KUZALIWA | URAIA | SIFA/ELIMU | TAREHE YA KUJIUNGA NAKAMPUNI |
|---|---|---|---|---|---|
| Bwn. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | 1969 | Mtanzania | Mchumi | 30.11.2018 |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 1943 | Mtanzania | Mchumi | 30.11.2018 |
| Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 1964 | Mtanzania | Mhasibu | 30.11.2018 |
| Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 1954 | Mtanzania | Kilimo/Mchumi | 30.11.2018 |
| Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 1968 | Mtanzania | Mchumi | 30.11.2018 |
| Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 1966 | Mtanzania | Mauzo na Manunuzi | 02.09.2019 |
| Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe | 1961 | Tanzanian | Teknohama | 30.09.2019 |


## UTAWALA BORA

Kanuni ya Kampuni inaitaka Bodi kuwa na Wajumbe saba (7) na wasipungue watano (5). Mwaka 2020, wajumbe wa Bodi walikuwa saba (7). Hakuna Mjumbe yoyote wa Bodi ambaye ni mfanyakazi wa Kampuni. Bodi inasimamia shughuli zote za Kampuni. Pamoja na mambo mengine, Bodi inaainisha athari zinazoweza kujitokeza katika shughuli za Kampuni, kutafuta njia za kuzuia katika kufanya maamuzi ya uwekezaji. Bodi inahakikisha taratibu zote katika utendaji wa Kampuni zipo na zinafuatwa kulingana na kanuni za utawala bora.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Disemba 31, 2020, Bodi ilikutana mara saba (7), ambapo Vikao vya kawaida vilikuwa vinne (4) na vikao maalum vitatu (3). Shughuli za kila siku za Kampuni zinasimamiwa na Afisa Mtendaji Mkuu akisaidiwa na wafanyakazi walioko chini yake. Kamati ya usimamizi pia huwa inaalikwa kuhudhuria vikao vya Bodi ili kuimarisha ufanisi katika shughuli za Kampuni na Utawala bora. Lengo la kufanyika kwa vikao maalum, ni pamoja na kujadili na kuidhinisha taarifa ya mahesabu ya kampuni yaliyokaguliwa.

## WAJUMBE WA BODI KWA MWAKA 2020, NA IDADI YA VIKAO WALIVYOHUDHURIA.

### WAJUMBE WA BODI KWA MWAKA 2020




| Na. | Jina | Nafasi | Idadi ya Vikao | Idadi ya Vikao Alivyohudhuria |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bwn. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | 7 | 7 |
| 2. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 7 | 7 |
| 3. | Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 7 | 7 |
| 4. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 7 | 7 |
| 5. | Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 7 | 6 |
| 7. | Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe | 7 | 6 |
| 8. | Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 7 | 7 |

Wajumbe wote wa Bodi wana sifa na uzoefu unaojitegemea ambao unasaidia katika kufanya maamuzi. Wajumbe wote hufuata Utawala Bora katika kufanya maamuzi. Wajumbe wa Bodi wanatambua na kufuata Kanuni za Utawala Bora.

Kwa mwaka wa fedha wa 2020, ili kutimiza kanuni za Utawala Bora, Bodi iliunda kamati mbili ambazo zilikutana kujadili mambo yahusianayo na shughuli za Kampuni. Kamati hizo ni:-

- Kamati ya Uwekezaji ambayo ina wajumbe watatu.
- Na kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ambayo ina wajumbe watatu.

### WAJUMBE WA KAMATI YA UWEKEZAJI:

| | WAJUMBE WA KAMATI YA UWEKEZAJI: | |
|---|---|---|
| 1. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Mwenyekiti |
| 2. | Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe |
| 3. | Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe |

Kamati ya Uwekezaji ilikutana mara nne (4) kujadili taarifa ya Kampuni ya kila robo mwaka, Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na Mpango Mkakati na Bajeti ya Kampuni kabla ya kuwasilisha kwenye Bodi kwa majadiliano na kufanya maamuzi.

### WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: -

| | WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: - | |
|---|---|---|
| 1. | Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mwenyekiti |
| 2. | Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe |
| 3. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe |

Kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ilikutana mara saba (7) kujadili Taarifa ya ndani ya Kampuni inayoandaliwa na Mkaguzi wa ndani na pia kupitia mahesabu ya Kampuni ya Mwaka mzima kabla na baada ya kukaguliwa.

### MAJUKUMU YA BODI KWA MWAKA 2020

Pamoja na Kusimamia shughuli za Bodi kwa mwaka 2020, Bodi ina majukumu yafuatayo:-

- Kuhakiki Taarifa za wanahisa wa Kampuni;
- Kupitia taarifa ya Kampuni iliyoandaliwa na Mkaguzi wa ndani;
- Kutafuta njia mbalimbali za kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni na kuongeza mapato;
- Kuandaa mpango mkakati na kupitisha bajeti ya mwaka 2021;
- Kufanya Upembuzi yakinifu na kukuza mapato ya Kampuni.

### IDADI YA HISA ZINAZOMILIKIWA NA WAJUMBE WA BODI KWENYE KAMPUNI

Idadi ya Hisa za kila Mjumbe wa Bodi ni kama ifuatavyo:-

| NA. | JINA | IDADI YA HISA ANAZOMILIKI |
|---|---|---|
| 1. | Prof. Lucian Ambrose Msambichaka | 487,580 |
| 2. | Bwn. Joseph Matanga Kahungwa | 40,600 |
| 3. | Bwn. Nathan Edward Mnyawami | 19,675 |
| 4. | Bi. Magdalene Nelson Enock Mkocha | 102,363 |
| 5. | Bwn. Paul F. Koyi ** | 830,498 |
| 6. | Bwn. Fortunatus Magambo** | 28,100,300 |
| 7. | Bwn. Mr. Ernest R. Khisombi ** | |

** Bwn. Paul F. Koyi: Alihudumu kwenye Bodi mwaka 2020 kwa nafasi yake ya Rais wa TCCIA ya kuiwakilisha TCCIA Makao Makuu ya Ofisi na Matawi yake zilizoko Mikoa yote ya Tanzania ambao wanamiliki jumla ya Hisa 830,213.
**Bwn. Fortunatus Magambo and Bwn. Ernest R. Khisombi kwa pamoja wanawakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) unaomiliki jumla ya Hisa 28,100,300.

**MTAJI WA KAMPUNI**

Mtaji wa Kampuni ulioidhinishwa ni Shilingi 100,000,000,000 ambavyo imegawanywa kwa mfumo wa hisa 5,000,000,000 ambapo kufikia Desemba 31, 2020 thamani ya hisa moja ilikuwa sawa na Shilingi 20. Hisa zilizokuwa zimelipiwa ni sawa na Shilingi 1,459,153 sawa na hisa 72,957,660 zenye thamani ya Shilingi 20 kila moja.

**Mgawanyiko wa Mtaji wa Kampuni na Umiliki wake.**

Hakuna mabadiliko yoyote kuhusu umiliki wa hisa kwa asilimia au katika mgawanyiko wa idadi ya hisa. Mgawanyiko huu wa hisa za Kampuni ni kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:-

| | 2018 | 2019 | 2018 | 2019 | 2018 | 2019 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Up to 28,100,300 | 1 | 1 | 38.50% | 38.50% | 28,100,300 | 28,100,300 | 562,006,000.00 | 562,006,000.00 |
| 1,700,001 -4,300,000 Shares | 1 | 1 | 5.80% | 5.80% | 4,215,000 | 4,215,000 | 84,300,000.00 | 84,300,000.00 |
| 1,600,001 -1,700,000 Shares | 1 | 1 | 2.30% | 2.30% | 1,686,000 | 1,686,000 | 33,720,000.00 | 33,720,000.00 |
| 1,250,001-1,600,000 Shares | 1 | 1 | 1.90% | 1.90% | 1,405,000 | 1,405,000 | 28,100,000.00 | 28,100,000.00 |
| 1,200,001 -1,250,000 Shares | 1 | 1 | 1.70% | 1.70% | 1,236,400 | 1,236,400 | 24,728,000.00 | 24,728,000.00 |
| 800,001 -1,200,000 Shares | 1 | 1 | 1.50% | 1.50% | 1,123,975 | 1,123,975 | 22,479,500.00 | 22,479,500.00 |
| 600,001 -800,000 Shares | 1 | 1 | 0.90% | 0.90% | 674,375 | 674,375 | 13,487,500.00 | 13,487,500.00 |
| 300,001 -600,000 Shares | 7 | 7 | 3.70% | 3.70% | 2,692,424 | 2,692,424 | 53,848,480.00 | 53,848,480.00 |
| 100,001 -300,000 Shares | 52 | 52 | 11.97% | 11.97% | 8,746,222 | 8,746,222 | 174,924,440.00 | 174,924,440.00 |
| 50,001 -100,000 Shares | 117 | 117 | 9.60% | 9.60% | 7,048,046 | 7,048,046 | 140,960,920.00 | 140,960,920.00 |
| 20,001 -50,000 Shares | 168 | 168 | 6.70% | 6.70% | 4,872,576 | 4,872,576 | 97,451,520.00 | 97,451,520.00 |
| 10,001 -20,000 Shares | 297 | 297 | 5.60% | 5.60% | 4,079,546 | 4,079,546 | 81,590,920.00 | 81,590,920.00 |
| 5,001 -10,000 Shares | 535 | 535 | 4.60% | 4.60% | 3,338,308 | 3,338,308 | 66,766,160.00 | 66,766,160.00 |
| 1,001 -5,000 Shares | 1508 | 1508 | 4.90% | 4.90% | 3,596,198 | 3,596,198 | 71,923,960.00 | 71,923,960.00 |
| 501 -1,000 Shares | 143 | 143 | 0.20% | 0.20% | 131,170 | 131,170 | 2,623,400.00 | 2,623,400.00 |
| 101 -500 Shares | 377 | 337 | 0.20% | 0.20% | 110,474 | 110,474 | 2,209,480.00 | 2,209,480.00 |
| 51 -100 Shares | 212 | 212 | 0.03% | 0.03% | 20,150 | 20,150 | 403,000.00 | 403,000.00 |
| 1-50 Shares | 3 | 3 | 0.00% | 0.00% | 92 | 92 | 1,840.00 | 1,840.00 |

**Mtaji wa Kampuni na Umiliki wake**

Kufikia Disemba 31, 2019, mtaji wa Kampuni uliolipiwa ulikuwa sawa na Shilingi 1,459,153,000. Kufikia tarehe 31 Disember, 2020 mtaji wa Kampuni uliongezeka na kufikia Shilingi 28.86 bilioni ambapo ni sawa na mara 19.8 ukilinganisha na mtaji wa Kampuni ambao thamani ya hisa ilikuwa sawa na Shilingi 385 kwa kila hisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2019. Kampuni iliorodhesha hisa zake kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam mwaka 2018.

Mtiririko wa Hisa za Kampuni kutoka tarehe 31 Disemba, 2020, 2019, 2018 na 2017

| Maelezo | 2020 | 2019 | 2018 | 2017 |
|---|---|---|---|---|
| Mtaji Kampuni Ulioidhinishwa (Shs) | 100,000,000,000 | 100,000,000,000 | 100,000,000,000 | 100,000,000,000 |
| Mtaji uliolipiwa (Shs) | 1,459,153,200 | 1,459,153,200 | 1,459,153,200 | 1,421,848,000 |
| Idadi ya Hisa zilizolipiwa sawa na Shs 20 | 72,957,660 | 72,957,660 | 72,957,660 | 71,092,400 |
| Mtaji wa Kampuni (Shs) | 26,858,704,000 | 28,260,507,000 | 28,260,507,000 | 30,051,788,000 |
| Mtaji wa Soko (Shs) | 28,088,699,100 | 28,088,699,100 | 28,088,699,100 | Nill |


Utendaji wa Kampuni kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2020
Kwa mwaka wa fedha wa 2020, mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia 40% na kufikia Shilingi 2.5 bilioni ukilinganisha na mwaka 2019. Ongezeko hili lilitokana na uamuzi wa Bodi wa kuuza baadhi ya hisa ambazo Kampuni inamiliki na kuwekeza katika Amana za Serikali kati ya mwaka 2019 na 2020.
Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2020, Kampuni ilipata hasara ya Shilingi 475 millioni. Hili ni anguko la asilimia 215 ukilinganisha na faida ya Shilingi 409 million kwa mwaka 2019. Hii imetokana na matakwa ya sheria mpya ya ukaguzi wa kimataifa (IFRs) 9 iliyopelekea hasara ya shilingi 1.35 billioni (operating loss) kutokana na mauzo ya hisa 450,000 za kampuni ya TBL zenye thamani ya shilingi 10,900 kwa hisa  kwa bei ya  shilingi 8,000 kwa hisa moja. Ikumbuwe kwamba hisa hizi zilinunuliwa kwa shilingi 2,060 mwaka 2012. Mauzo yaliyotokana na mauzo haya (shilingi 3.6 billioni) yamewekezwa kwenye hatifungani za serikali ili kupanua wigo na uhakika wa mapato.

## KULIPA GAWIO

Kwa mwaka wa fedha 2020 Bodi inapendekeza gawio la shilingi 6 kwa hisa ambalo ni sawa na gawio la mwaka jana 2019.

## USAWA WA KIJINSIA KAZINI

Kampuni inazingatia usawa wa kijinsia katika kuajiri wafanyakazi wake na haina ubaguzi katika utendaji wake. Kufikia Desemba 31, 2020, wafanyakazi wa Kampuni walikuwa kama ilivyoainishwa na jinsia zao kwenye jedwali hapa chini:




| | 31 - DIS | 31 - DIS |
|---|---|---|
| Jinsia | 2020 | 2019 |
| Wanaume | 2 | 4 |
| Wanawake | 2 | 2 |
| **Jumla** | **4** | **6** |

## MASLAHI YA WAFANYAKAZI

Kampuni inawapa wafanyakazi wake maslahi yafuatayo:

### Elimu

Kampuni inawafadhili wafanyakazi wake kujiendeleza kielimu katika kozi za muda mfupi ndani na nje ya nchi kwa taaluma mbalimbali kulingana na uhitaji na kiwango cha fedha kinachohitajika. Kampuni pia inasaidia wafanyakazi pale wanapoamua kujiendeleza wenyewe kwa masomo ya muda mrefu.

### Mkopo kwa Wafanyakazi

Kampuni inatoa mikopo kwa wafanyakazi ya muda mrefu na mfupi kuweza kutatua matatizo ya kifedha na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi za kujiongezea kipato. Mikopo hiyo inatolewa kulingana na masharti yaliyowekwa na Bodi na inatolewa kulingana na Bajeti ya mwaka.

### Huduma ya Matibabu

Kampuni imeingia mkataba na Shirika la Bima ya Afya la Taifa (NHIF) kutoa huduma ya afya kwa wafanyakazi wa Kampuni na wategemezi wao.

### Msaada wa Kifedha

Kampuni inaandaa sera ya kusaidia pale mfanyakazi anapofariki au wategemezi.

### Mafao ya Kustaafu

Kampuni inachangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PSSSF na NSSF) kwa ajili ya mafao ya baadaye kwa wafanyakazi wake.

### Watu wasiojiweza (Walemavu wa Viungo)

Kampuni inatoa nafasi sawa ya ajira kwa watu wote yaani wenye viungo vyote na wale wenye ulemavu wa viungo.

### KUKIDHI MATAKWA YA KISHERIA

Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau wake. Lakini pia Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa (DSE), Madalali wa Soko la Hisa (Brokers) na Benki za Biashara. Kwa mwaka 2020, Kampuni imeweza kutimiza taratibu na vigezo vyote kulingana na Matakwa ya Mamlaka husika.

## UDHIBITI WA ATHARI ZA UTAWALA WA NDANI YA KAMPUNI

Bodi ina wajibu wa kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza katika utendaji kwenye Kampuni. Kamati ya usimamizi inahakikisha kuwa kunakuwa na fedha za kutosha na mfumo wa ufanyaji kazi katika Kampuni unazingatiwa. Lengo la Kampuni ni:

- Kulinda stahiki za wanahisa na mali ya Kampuni.
- Ufanisi na Ubora katika kazi;
- Kukidhi matakwa ya Mamlaka na Sheria.
- Kuwepo kwa rekodi ya Mahesabu na Taarifa ya Fedha.
- Kampuni kuendelea na shughuli za utendaji katika mazingira ya kawaida na yasiyo ya kawaida.
- Kuwajibika kwa wadau wa Kampuni.

Ufanisi na udhibiti wa mfumo wowote wa utendaji wa ndani unategemea utaratibu wa hatua zilizochukuliwa. Kuna athari zinazoweza kujitokeza kwa kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa wafanyakazi. Mfumo wa ndani wa Kampuni una lengo la kuwahakikishia wakurugenzi, kazi zinafanyika kwa ufanisi. Wakurugenzi wana mamlaka ya kufuatilia mfumo wa ndani wa utendaji na kujiridhisha.

Kampuni ina sera mbalimbali ambapo kupitia hizo inaweza kudhibiti athari kwenye Kampuni. Na kwa upande mwingine, Kampuni imemwajiri Mkaguzi wa ndani wa muda ambaye anasimamiwa na Bodi kupitia Kamati ya Ukaguzi ambapo kupitia yeye Bodi inaweza kusimamia utendaji wa Kampuni kwa ufanisi mkubwa.

Tathmini na Athari za Kampuni na Namna ya Kuzizuia.

Kampuni imewekeza katika taasisi za fedha ikiwemo Amana za serikali za muda mfupi na muda mrefu, Amana za Makampuni, mikopo, amana za mabenki na kwenye hisa. Maeneo mengine ya uwekezaji ni pamoja na biashara zinazotoa faida. Lengo la uwekezaji huu ni kuongeza mapato kwenye Kampuni.

Athari zinazoweza kuikumba kampuni ni pamoja na: -

### Athari za Kutopata Faida

Hii inatokana na mwenendo wa Hisa katika Soko la Hisa ambapo hisa za makampuni ambayo Kampuni inamiliki hisa zimeshuka thamani. Uwekezaji katika Amana za Serikali kipato chake ni cha uhakika na husaidia kupunguza athari ya

kukosa faida katika Kampuni.

### Athari katika Ubadilishaji wa Fedha

Hii ni athari inayojitokeza wakati wa ubadilishaji wa fedha za kigeni. Hii haiathiri sana Kampuni kwa sababu kwa sasa hatuna biashara inayotupelekea kubadilisha fedha.

### ATHARI ZA MIKOPO

Hii inatokana na upande mmoja kushindwa kutimiza wajibu wake wa kulipa deni kwa tarehe inayopangwa. Ili kupunguza hii athari, Kampuni imeandaa sera ya uwekezaji kutathmini kabla ya kufanya uwekezaji na ngazi za uidhinishaji katika kila eneo la uwekezaji.

### Athari ya Hisa Kushindwa Kuuzwa

Hii athari inatokana na kushindwa kufikia malengo. Lakini pia hii athari inatokana na kushindwa kuuza hisa kwa wakati na kwa bei iliyokusudiwa. Kampuni inaweza kupunguza hii athari kwa kuwekeza kwenye amana za benki za muda mfupi zinazoweza kukamilisha mipango yake ya uwekezaji na matumizi ya ndani ya Kampuni. Kampuni imekuwa ikifanya makisio ya mapato na matumizi ya kila mwezi. Kampuni inategemea kipato chake kikubwa toka kwenye Magawio kutoka kwenye Makampuni inayomiliki hisa na maeneo mengine ilikowekeza.

### Athari za Kiutendaji

Hii inatokana na mfumo duni, usimamizi dhaifu, utendaji dhaifu, udanganyifu katika kazi, wizi na makosa mengine ya kibinadamu. Kampuni inajitahidi kuiepuka hii athari kwa kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa ndani wa Kampuni. Moja ya mbinu za kudhibiti ni pamoja na kufuata miongozo ya kiutendaji na taratibu zilizowekwa, sera na miongozo na kuajiri Mkaguzi wa ndani wa muda. Kusimamia athari za kiutendaji katika Kampuni ni muhimu katika shughuli za kila siku. Kamati ya usimamizi, Mkaguzi wa Ndani wa muda, Kamati ya Uwekezaji, Kamati ya Ukaguzi na Bodi ya Wakurugenzi wanahusika kikamilifu katika usimamizi wa Kampuni.

### Athari za Rasilimali Watu

Kulingana na uhalisia wa shughuli za Kampuni, inahitaji wafanyakazi wenye nidhamu na wenye maarifa maalum katika maeneo muhimu ya kiutendaji. Muundo wa Wafanyakazi wa Kampuni unaisaidia Kampuni kuingiza mapato makubwa. Ili kuhakikisha athari hii ya rasilimali watu inazuiwa, Kampuni inahakikisha inawekeza kwa wafanyakazi wake, kupitia kuboresha maslahi yao kila mara.

### Athari ya kampuni Kupoteza Sifa yake Nzuri

Kampuni ina wajibu wa kuhakikisha majukumu yake yanafanyika vizuri ili kulinda sifa yake katika makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa kulingana na sheria na taratibu husika. Katika kuhakikisha hili linafanyika, Bodi na kamati ya usimamizi inahakikisha inatimiza wajibu wake kwa kuzingatia sheria za utawala bora na kwa kuzingatia utendaji bora.

### Kulinda Mali za Kampuni

Wakurugenzi wana wajibu wa kulinda mali ya Kampuni. Bodi imeidhinisha baadhi ya sera na kanuni lakini haizuiliwi na taratibu za fedha, sera ya uwekezaji ili kuimarisha mazingira ya utendaji wa ndani. Hizi sera zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya mazingira ya kiutendaji. Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kutoa taarifa kwamba hakuna udanganyifu wowote uliofanyika kwa mwaka wa fedha wa 2020.

Upatikanaji wa Taarifa ya Mahesabu na Taarifa ya Fedha

Kampuni ina wafanyakazi wenye uzoefu katika kitengo cha uhasibu na fedha. Vitabu vya mahesabu vimekuwa vikitunzwa na taarifa ya fedha inaandaliwa kulingana na Sheria ya Kimataifa ya Uandaaji wa taarifa za Mahesabu. (IFRS).

## MIPANGO YA BAADAYE

Kuanzia mwaka 2018, Bodi ya Wakurugenzi iliamua kupunguza uwekezaji wake kwenye hisa na kuwekeza maeneo mengine ambayo ilikuwa bado haijawekeza. Toka Kampuni imeanza kufanya shughuli za biashara Oktoba, 2005 zaidi ya asilimia tisini na tano (95%) ya uwekezaji wake ilikuwa ni kwenye hisa za makampuni yaliyoorodhesha hisa zake kwenye Soko la Hisa. Bodi iliamua kuwekeza kwenye maeneo yenye mapato ya uhakika (Amana za Serikali, Amana za Makampuni na faida inayotokana na Amana za Mabenki). Bodi ya Wakurugenzi inaamini kuwa kuwekeza katika taasisi hizi za kifedha ni biashara nzuri kwa kuzingatia pale ambapo Soko la Hisa litashindwa kufanya vizuri kama ilivyo sasa ambapo kipato chake hakitabiriki. Bodi ya Wakurugenzi imeamua kuelekeza uwekezaji wake kwenye amana za serikali kwa sababu faida yake ni ya uhakika ukilinganisha na uwekezaji katika hisa.

Mwisho, Bodi inapenda kuainisha maeneo mengine ya uwekezaji kama kuagiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, wakala wa huduma ya bima, usindikaji wa mazao na maeneo mengine ya taasisi ya fedha kama ubadilishaji wa fedha za kigeni.

## MTAZAMO WA BODI

Bodi ya Wakurugenzi inatazamia taarifa ya Mahesabu kutoa picha kamili ya masuala ya kifedha ya Kampuni kama ilivyokuwa kufikia tarehe 31 Desemba, 2020 na faida/ hasara na mzunguko wa kifedha kwa mwaka kulingana na kanuni za uandaaji wa taarifa za mahesabu za Kimataifa na sheria ya makampuni ya mwaka 2002. Hata hivyo, hakuna chochote kinachoipa mashaka Bodi kwamba Kampuni itashindwa kuendelea na shughuli zake za biashara kwa miezi kumi na mbili (12) ambayo tangu kutolewa kwa hii taarifa ya mahesabu.

## WAKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI

Wakaguzi wa Mahesabu, CROWE Tanzania, wameendelea kuonyesha nia yao ya kuendelea kukagua mahesabu ya Kampuni endapo watateuliwa tena kukagua mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha utakaoishia tarehe 31 Desemba, 2021. Hata hivyo, Bodi itawasilisha pendekezo la uteuzi wa mkaguzi katika dondoo zinazofuata.

Taarifa hii imeidhinishwa na Bodi katika Mkutano maalum uliofanyika tarehe 25/06/2021 na kusainiwa na wajumbe wafuatao:

| | |
|---|---|
| **Prof. Lucian A. Msambichaka** | **Bwn. Joseph M. Kahungwa** |
| Mkurugenzi | Mkurugenzi |
| Tarehe:**12/05/2021** | Tarehe:**12/05/2021** |

## WAJIBU WA WAKURUGENZI

Kulingana na sheria ya makampuni ya mwaka 2002, Wakurugenzi wana jukumu la kuandaa Taarifa ya mahesabu ya kila mwaka ambayo inatoa picha halisi ya Kampuni kila mwisho wa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli za Kampuni. Wakurugenzi wana wajibu wa kutunza kumbukumbu za Mahesabu ya Kampuni ambayo inaeleza kwa uwazi kuhusu mwelekeo wa Kampuni. Wakurugenzi wana wajibu wa kusimamia na kulinda mali za Kampuni.

Ili kuwawezesha wakurugenzi kufikia malengo haya, wanatakiwa kuweka mikakati ya kupunguza au kuondoa kabisa hasara kwa gharama yoyote. Hii inajumuisha mpangilio wa majukumu, na mgawanyo wa kazi. Wafanyakazi wote wanapaswa kudumisha kiwango cha juu cha maadili ili kuhakikisha kazi zinafanyika kwa usahihi na kuondoa mazingira yoyote yanayoweza kuisababishia Kampuni hasara.

Wakurugenzi wana wajibu wa Kuandaa Taarifa ya mahesabu ya Kampuni ya mwaka mzima, ambayo yanaandaliwa kulingana na Sera ya Uandaaji wa Taarifa za Mahesabu.

Jukumu hili ni pamoja na kubuni, kutekeleza, na kudumisha udhibiti wa ndani unaofaa kwa uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha ambazo ni sahihi kwa kutumia Sera za Uandaaji wa Mahesabu, na kufanya makadirio kulingana na mazingira yaliyopo.

Wakurugenzi wana wajibu wa kuandaa taarifa ya mahesabu, kulingana na sera ya Uandaaji wa Mahesabu Pamoja na Sheria ya Kimataifa ya Uandaaji wa taarifa za kifedha na matakwa ya Sheria za Makampuni ya mwaka 2002. Wakurugenzi wana wajibu wa kusimamia na kuwasilisha taarifa ya fedha kwa usahihi.

Wakurugenzi wanaamini kuwa taarifa ya Mahesabu inatoa picha kamili ya masuala ya kifedha ya Kampuni na matokeo ya kiutendaji. Wakurugenzi wanakubali jukumu la utunzaji wa kumbukumbu za Mahesabu na jukumu zima la uandaaji wa taarifa za Mahesabu. Wakurugenzi wana wajibu wa kusimamia na kudhibiti mfumo wa ndani wa kifedha uliowekwa na Kampuni.

Hata hivyo, hakuna chochote kinachoipa mashaka Bodi kwamba Kampuni itashindwa kuendelea na shughuli zake za biashara kwa miezi kumi na mbili (12) tangu kutolewa kwa taarifa hii ya mahesabu.

**Prof. Lucian A. Msambichaka**
Mkurugenzi
Tarehe:**12/05/2021**

**Bwn. Joseph M. Kahungwa**
Mkurugenzi
Tarehe:**12/05/2021**

## UTHIBITISHO WA MKUU WA IDARA YA UHASIBU

Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu (NBAA) kulingana na uwezo wake katika kuwapima na kusajili Wahasibu na wakaguzi wa mahesabu Pamoja na sheria ya makampuni namba thelathini na tatu (33) ya mwaka 1972, na kurekebishwa na Sheria namba mbili (2) ya mwaka 1995, inaitaka Taarifa ya mahesabu kuambatanishwa na uthibitisho kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Fedha/ Mahesabu aliyehusika kuaanda taarifa ya Fedha ya Kampuni husika. Mtaalam wa Mahesabu anapaswa kuwasaidia Wakurugenzi/ Wafanyakazi kutekeleza jukumu la kuandaa taarifa za kifedha za taasisi inayotoa picha halisi ya Kampuni na utendaji wake kulingana na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa na matakwa ya kisheria ya uandaaji wa taarifa za kifedha.
Jukumu kamili la kisheria kwa utayarishaji wa taarifa za kifedha liko kwa Bodi ya Wakurugenzi kama ilivyoonyeshwa hapo juu kwenye Wajibu wa Wakurugenzi

Mimi Joel Chikoma, nikiwa ni Mkuu wa idara ya Uhasibu ya TCCIA INVESTMENT PLC ninathibitisha kwamba, Taarifa ya Mahesabu ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2020 imeandaliwa kulingana na Viwango vya Uhasibu na Matakwa ya Kisheria. Ninathibitisha kwamba, Taarifa ya Mahesabu inatoa picha kamili ya TCCIA INVESTMENT PLC kufikia tarehe hiyo iliyotajwa hapo juu na kwamba zimeandaliwa kulingana na taarifa za kifedha zinazotunzwa vizuri.

**Joel Chikoma**
Mkuu wa Idara ya Uhasibu na Uwekezaji
NBAA Membership No: ACPA 3285
Tarehe:**12/05/2021**

# MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2020

TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA WA FEDHA ULIOISHA 31/12/2020

| | 2020 Shilingi '000 | 2019 Shilingi '000 |
|---|---|---|
| Mapato | 2,507,571 | 1,787,692 |
| Mapato anuwai | 13,360 | - |
| Mapato mengine/ (hasara) ya uendeshaji | (1,347,870) | (88,410) |
| Matumizi ya uendeshaji | (1,060,243) | (1,061,732) |
| **Faida ya uendeshaji** | **112,818** | **637,550** |
| Gharama za mtaji | (466,557) | (16,638) |
| **Faida/ (hasara) kabla ya kodi** | **(353,739)** | **620,912** |
| Kodi | (121,397) | (211,198) |
| **Faida/(Hasara) kwa mwaka** | **(475,136)** | **409,714** |
| **Mapato mengine kamili** | | |
| Kupanda/ (kushuka) kwa thamani ya hisa | 388,225 | (1,688,114) |
| **Mapato/(hasara) mengine ya mwaka** | **388,225** | **(1,688,114)** |
| **Jumla ya mapato/(hasara) kwa mwaka** | **(86,911)** | **(1,278,400)** |
| **Mapato kwa kila hisa** | **(6.51)** | **5.62** |

## TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI 31/12/2020

| | 2020 | 2019 |
|---|---|---|
| **Rasilimali** | **Shilingi' 000** | **Shilingi' 000** |
| **Rasilimali za muda mrefu** | | |
| Mali ya kudumu inayogusika | 26,307 | 21,456 |
| Haki ya matumizi ya rasilimali | 42,316 | - |
| Uwekezaji wa kwenye ardhi/majengo | 221,347 | 239,820 |
| Uwekezaji wa kwenye hisa | 14,848,114 | 19,364,888 |
| Dhamana za serikali | 13,578,175 | 9,677,922 |
| Kodi iliyoahirishwa | - | 1,605 |
| Amana za makampuni/mashirika | - | 30,336 |
| Uwekezaji mwingine | - | 5,500 |
| | **28,716,259** | **29,341,527** |
| **Rasilimali za muda mfupi** | | |
| Rasilimali za biashara | 571,177 | 406,964 |
| Kodi ya muda mfupi | 273,350 | 340,051 |
| Amana za makampuni/mashirika | 10,000 | - |
| Fedha na thamani ya fedha | 206,233 | 224,314 |
| | **1,060,760** | **971,329** |
| **Jumla ya Rasimali** | **29,777,019** | **30,312,856** |
| | | |
| **Mtaji na Madeni** | | |
| **Mtaji** | | |
| Mtaji | 2,167,952 | 2,167,952 |
| Jumla ya akiba | 5,430,850 | 9,020,625 |
| Faida kuu | 18,972,207 | 15,907,804 |
| | **26,571,009** | **27,096,381** |
| | | |
| **Mdeni ya muda mrefu** | | |
| Mkopo wa muda mrefu | | 2,789,285 |
| Kodi iliyoahirishwa | 3,256 | - |
| | | **2,789,285** |
| **Madeni ya muda mfupi** | | |
| Madeni ya biashara | 151,075 | 44,289 |
| Dhima ya kukodisha | 39,093 | - |
| Mkopo wa muda mfupi | 183,092 | 210,715 |
| Gawio | 223,301 | 172,186 |
| | **596,561** | **427,190** |
| **Jumla ya madeni** | **3,206,010** | **3,216,475** |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **29,777,019** | **30,312,856** |

Taarifa hii ya mahesabu ilithibitishwa kwa ajili ya kutangwazwa na Bodi na ilisainiwa kwa niaba yao na :

**Bw. Fortunatus Makore Magambo**
Mwenyekiti
Tarehe:**12/05/2021**

**Prof. Lucian Msambichaka**
Mjumbe
Tarehe:**12/05/2021**

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA 2020

| | Mtaji wa hisa | Mapato ya hisa | Jumla ya mtaji wa hisa | Akiba ya thamani ya uwekezaji kwenye hisa | Gharama ya IPO | Faida kuu | Jumla ya mtaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Shilingi '000** | **'000** | **'000** | **'000** | **'000** | **'000** | **'000** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 01/01/2019** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **(2,030,139)** | **(629,662)** | **28,866,630** | **28,374,781** |
| Faida ya mwaka | | | | | | 409,714 | 409,714 |
| Mapato mengine | - | | | 11,515,426 | - | - | 11,515,426 |
| Kuhamisha kwenda akiba kuu | | | | 165,000 | | (13,368,540) | (13,203,540) |
| **Usawa tarehe 31/12/2019** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **9,650,287** | **(629,662)** | **15,907,807** | **27,096,381** |
| **Muda wa sasa:** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 01/01/2020** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **9,650,287** | **(629,662)** | **15,907,807** | **27,096,384** |
| Hasara ya mwaka | | | | | | | (475,136) |
| Mpato mengine | | | | 388,225 | | | 388,225 |
| Kuhamisha kwenda akiba kuu | | | | (3,978,000) | | | - |
| Gawio | | | | | | | (438,464) |
| | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 31/12/2020** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | **6,060,512** | **(629,662)** | **18,972,207** | **26,571,009** |

## TAARIFA YA MZUNGUKO WA FEDHA

| | 2020 | 2019 |
|---|---|---|
| | **Shilingi '000** | **Shilingi '000** |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uendeshaji** | | |
| | | |
| Fedha iliyotoka kwenye shughuli za uendeshaji | 1,461,036 | 480,238 |
| Gharama za kifedha | (466,557) | (16,638) |
| Kodi iliolipwa | (49,835) | (50,743) |
| **Fedha taslimu inayotokana na uendeshaji** | **944,644** | **412,857** |
| | | |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uwekezaji** | | |
| | | |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | (11,600) | (3,960) |
| Mauzo ya mali ya kudumu inayogusika | - | 1,588 |
| Manunuzi ya haki ya kutumia rasilimali | (74,866) | - |
| Mzunguko kwenye uwekezaji katika hisa | 4,904,999 | 1,935,000 |
| Manunuzi ya dhamana za serikali | (3,900,253) | (5,428,683) |
| Mzunguko kwenye amana za makampuni | 20,336 | 28,370 |
| Hasara kwenye uuzaji wa hisa | (1,342,370) | (82,120) |
| **Fedha taslimu iliotumika katika uwekezaji** | **(403,754)** | **(3,549,805)** |
| | | |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na mtaji** | | |
| | | |
| Mzunguko wa mkopo | (210,715) | 3,000,000 |
| Mzunguko wa dhima ya kukodisha | 39,093 | - |
| Gawio lililolipwa | (387,349) | (289,587) |
| **Fedha taslimu iliotokana na mtaji** | **(558,971)** | **2,710,413** |
| | | |
| **Jumla ya fedha taslimu za mzunguko kwa mwaka** | (18,081) | (426,535) |
| Fedha na thamani ya fedha mwanzo wa mwaka | 224,314 | 650,849 |
| **Fedha na thamani ya fedha mwisho wa mwaka** | **206,233** | **224,314** |

**WASILISHO:**

Ndugu Wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2020 na kuazimia kama ifuatavyo.



## "Azimio la 2/2021

Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2020 imepitishwa kama ilivyowasilishwa."

Dondoo Na. 16/5/2021

### KUTANGAZA GAWIO


Kwa mwaka wa fedha ulioshia Desemba,31 2020 Bodi inapendekeza kulipa gawio la shilingi 6 kwa hisa (2019: shilingi 6 kwa hisa).

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.

## Azimio la 3/2021

"Mkutano Mkuu umeazimia, kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania Sita (6) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi."




Dondoo Na. 16/6/2021

## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2020

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2020, Mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania. Hadi sasa Bodi imeridhika na kazi ambayo ilifanywa na Kampuni hii kwa mwaka 2020. Aidha Kampuni hiyo imeonyesha nia ya kuendelea kukagua Mahesabu ya Kampuni yetu kama watateuliwa tena.

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2021. Ada ya Ukaguzi inayopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 20 milioni Kabla ya kodi. Ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.



## "Azimio la 4/2021

Imeazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2021. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 20 milioni kama gharama za malipo ya ukaguzi wa Mahesabu ya Kampuni."


Dondoo Na. 16/7/2021

## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".
Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi. Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

### WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2020, Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000).



"**Azimio la 5/2021**

Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi."

Dondoo Na. 16/9/2021

## MABADILIKO KWENYE DAFTARI LA WANAHISA

Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) ilielekeza bodi kurekebisha kasoro kwenye daftari la Wanahisia. Kulingana na taarifa sahihi ya idadi za hisa zinazoonyeshwa kwenye taarifa ya hesabu za Kampuni ni 72,957,660, tofauti na taarifa zilizopo kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam ambazo ni 73,077,253, hii ikiwa ni tofauti ya hisa 119,593. Bodi pamoja na Menejimenti imepitia taarifa zote na kubaini uwepo wa Wanahisa watatu waliowekewa hisa hizo kimakosa ambao ni; TCCIA Mwanza, Francis Michael Masanja, and Jayant Vatshi Jethwa. Kampuni iliwasiliana na ofisi TCCIA Mwanza na wakashindwa kutoa udhibitiso wa Malipo, Mwanahisa Francis Michael Masanja aliwekewa hisa za ziada wakati likifanyika zoezi la kuunganisha vyeti vyake vya hisa wakati Jayant Vatshi Jethwa alikiri kutokuwa na hisa kwenye Kampuni

### UWASILISHAJI

Wanahisa wanaombwa kuridhia kurekebisha kasoro zilizojitokeza kwa kuondoa tofauti ya hisa 119,593 kati ya taarifa zilizopo kwenye hesabu za Kampuni na taarifa zilizopo Soko la Hisa la Dar es Salaam.

## "Azimio la 6/2021

Imeazimiwa kwamba mabadiliko yaliyopendekezwa kufanyika katika daftari la Wanahisa yafanyike kwa kuwaondoa TCCIA Mwanza na Jayant Vatshi Jethwa kwenye daftari la Wanahisa Pamoja na kurekebisa taarifa za Mwanahisa Francis Michael Masanja ."

Dondoo Na. 16/10/2021

# UCHAGUZI WA WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI 2021

## 1. UTANGULIZI

1.1. Kifungu Namba 69 cha Katiba ya Kampuni, kinatamka kuwa idadi ya Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi itakuwa si chini ya 5 wala haitazidi 7 kama ifuatavyo:.

1.1.1. Kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma utengewe nafasi mbili kwa kuwa PSSSF inamiliki asilimia 38.52 ya hisa za Kampuni.

1.1.2. Chemba ya Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Kilimo itengewe nafasi moja ambayo Mjumbe atakuwa ni Rais wa Chemba akiwasilisha Wanahisa wadogo ambao wengi ni wanachama wa Chemba.

1.1.3. Mjumbe mmoja achaguliwe kutoka Kundi la Wanataaluma. Mjumbe huyo atapigiwa kura na Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu.

1.1.4. Wajumbe watatu (3) wawe na sifa zilizotajwa hapo chini. Wajumbe hao watachaguliwa na wanahisa wadogo na kwamba PSSSF na Rais wa Chemba hawatawapigia kura.

## 2.0. SIFA ZA MWOMBAJI

I. Mwombaji awe ni Mwanahisa;

II. Mwombaji awe na elimu ya Chuo Kikuu kinachotambulika kitaifa au kimataifa, mwenye elimu ya uchambuzi na ufahamu wa kina katika masuala ya kitaaluma, hususan: Uhasibu, Kilimo, Biashara, Sheria, Uwekezaji, Uchumi, Fedha na Utawala;

III. Awe na uwezo wa kujieleza kwa Kiswahili na Kiingereza kwa ufasaha;

IV. Awe na uzoefu wa Ukurugenzi kwenye Bodi za makampuni, taasisi kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu;

V. Awe na umri wa miaka kumi na nane (18) au Zaidi.

## 3.0. HATUA ZILIZOCHUKULIWA

3.1. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuavyo:

I. Tarehe 24 Septemba, 2021 Tangazo lilitolewa kwa ajili ya kujaza nafasi nne zinazobaki baada ya kutenga nafasi zilizotengwa kwa ajili ya PSSSF na TCCIA na kwamba wanahisa wenye sifa pekee ndio wanatakiwa kuomba nafasi ya kuchaguliwa kuwa Wajumbe wa Bodi. Tangazo lilielekeza kwamba maombi yawasilishwe kabla ya tarehe 10 Novemba, 2021. Tangazo hili lilitangazwa kwenye gazeti la Daily News na kwenye tovuti ya kampuni .

II. Katika kuzingatia kuwa tathmini inafanyika kwa uhuru na haki Bodi iliteua Menejimenti kufanya tathmini ya maombi na kuwasilisha mapendekezo yake mbele ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa ajili ya uchaguzi. Maombi yaliyopelekewa ni yale yaliyowasilishwa kulingana na muda uliokuwa umewekwa kama inavyoonyeshwa kwenye Tangazo.

## 4.0. MWISHO

4.1. Mwisho Mkutano Mkuu unaombwa kupokea orodha ya Wajumbe waliokidhi vigezo kuwa Wajumbe wa Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu ijayo, kuanzia Desemba 2021. Baada ya hapo Mkutano Mkuu uhitimishe zoezi kwa kupiga kura.

I. Mkutano Mkuu upokee na kuridhia Wajumbe wawili walioteuliwa na PSSSF.

II. Mkutano Mkuu upokee na kuridhia uteuzi wa Ndugu Paul Koyi ambaye kwa sasa ni Rais wa Chemba ya Wafanya Biashara, Wenye Viwanda na Kilimo.

III. Wakati wa kupiga kura Mkutano Mkuu utaanza kumpigia kura Mjumbe Mmoja ambaye yuko kwenye Kundi la Wataalamu. Mjumbe huyu atapigiwa kura na Wanahisa wote pamoja na wale ambao wamehudhuria Mkutano kama wawakilishi walioteuliwa na wanahisa ambao hawakuweza kuhudhuria Mkutano (MWAKILISHI).

IV. Wakati wa kupiga kura, kila hisa moja ni sawa na kura moja.

Nawasilisha

**Katibu wa Bodi**

## UCHAGUZI WA MJUMBE MMOJA MTAALAMU

### NATHAN EDWARD MNYAWAMI – MIAKA 53

Bwana Mnyawami ana Shahada ya Uchumi kutoka Chuo Kikuu cha Makerere, 1993 na Shahada ya Uzamili ya Uchumi kutoka Chuo kikuu cha Dar es Salaam, 2002. Bwana Mnyawami ana uzoefu wa miaka 20 katika kazi. Kuanzia mwaka 1994 hadi 2002, alikuwa ameajiriwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) kama Mtakwimu chini ya Mkurugenzi wa Masoko na Uwekezaji. Oktoba, 2002 hadi 2015 alijiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Mashirika ya Umma (PPF) kama Mratibu/ Meneja wa Mipango na Utafiti. Alijiunga tena na TPDC mwaka 2015 kama Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji.

*Bwana Mnyawami ana uzoefu wa Zaidi ya miaka 10 kwenye Bodi mbalimbali. Na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).*

### OSWALD M. URASSA – MIAKA 57

Ana Shahada ya Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya Uzamili ya Biashata kutoka Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza. Bwana Urassa ana uzoefu wa miaka 30 katika kazi. Kuanzia mwaka 1991 hadi 1998 alikuwa ameajiriwa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kama Mwalimu Msaidizi chini ya Mhadhiri Mwandamizi. Mwaka 1999 hadi 2007 alikuwa ameajiriwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) kama Meneja wa Fedha na Uendeshaji. Mwaka 2007 hadi 2009 alikuwa ameajiriwa na Benki ya NMB kama Mkuu wa Idara ya Hazina kabla ya kupandishwa cheo na kuwa Mkuu wa Idara ya Mahusiano ya Wawekezaji mwaka 2009 hadi 2010. Kwa sasa ameajiriwa na Tanzania Mortage Refinance Company Ltd (TMRC) kama Mkuu wa Idara ya Fedha kuanzia 2011.

*Bwana Urassa ana uzoefu Zaidi ya miaka 10 kwenye Bodi. Na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).*

### THOMAS ENOCK – MIAKA 37

Ana Shahada ya Biashara ya Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya Uzamili ya Fedha kutoka Chuo kikuu cha South Wales. Bwana Enock alikuwa ameajiriwa na BancABC kuanzia 2009 hadi 2015 kama Mdhibiriti wa Uendeshaji wa Shirika na Utwala kabla ya kupandishwa cheo na kuwa Mkaguzi wa Ndani Desemba, 2011 hadi Julai, 2015. Kwa sasa ameajiriwa na Benki ya Mkombozi kama Mkuu wa Idara ya Mpango Mikakati na Maendeleo ya Biashara mwaka 2015 kabla ya kupandishwa cheo na kuwa Mkuu wa Idara ya Fedha Januari, 2020,, nafasi ambayo anaitumikia hadi sasa.

Bwana Thomas amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).

## UCHAGUZI WA WAJUMBE WATATU AMBAO NI WANAHISA

### PROF. LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA - MIAKA 78

Prof. Msambichaka ana Shahada ya Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Dar-s- Salaam, Shahada ya Uzamili na Uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Leipzig Ujerumani. Prof. Msambichaka ni Mjumbe wa Bodi zifuatazo: Jumuiya ya Uchumi ya Kilimo Tanzania, Jumuiya ya Uchumi Tanzania na Utawala na Usimamizi wa Umma katika Jumuiya ya Afrika. Na pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji. Prof. Msambichaka amewahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi wa mashirika kadhaa ikiwepo Bodi ya Wakurugenzi ya Ngozi Morogoro, Taasisi ya Fedha ya Maendeleo ya Biashara, Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa, Chuo Kikuu cha Biashara Moshi (MUCCOBS), Usajili wa Biashara na Utoaji wa Leseni [BRELA], Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Mto Rufiji (RUBADA), Chuo cha Ustawi wa Jamill na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC).

*Prof. Msambichaka ana uzoefu Zaidi ya miaka 10 kwenye Bodi. Na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).*

### BWANA JOSEPH MATANGA KAHUNGWA - MIAKA 57

Bwana Kahungwa ana shahada ya Biashara katika masuala ya Uhasibu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 1987, na shahada ya Uzamili katika Uongozi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, 2003. Pia yeye ni Makamu wa Rais (Kilimo) wa TCCIA tangu Mei 2013 mpaka sasa, mwanahisa na mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Uwekezaji ya TCCIA na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Ukaguzi. Bwana Kahungwa alikuwa Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mwanza (Machi 2008 hadi Machi 2013). Hali kadhalika, alikuwa Makamu Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mwanza (Machi 2001 hadi Machi 2008), Mjumbe wa Bodi ya CRDB Bank PLC kutoka mwaka 2001 hadi 2006, Mjumbe wa Kamati ya Fedha ya Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT) kutoka 1977 hadi 2014. Awali, alikuwa na nyadhifa kama vile Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Pangea Minerals Ltd kutoka Julai 1999 hadi 2001, Mhasibu Mwandamizi - Pangea Minerals Ltd, Mhasibu Mwandamizi na Msimamizi wa Mikopo – Bodi ya Biashara ya Nje kutoka 1992 hadi 1994. Pia alikuwa Mhasibu wa Bodi hiyo kutoka 1991 hadi 1992.
*Bwana Kahungwa ana uzoefu Zaidi ya miaka 10 kwenye Bodi. Na pia amesajiliwa na na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).*

### BI. MAGDALENE NELSON ENOCK MKOCHA - MIAKA 67

Bi Mkocha ana shahada ya Sayansi katika Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, 1979, na shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. 1988. Ana uzoefu wa kufanya kazi wa miaka 37. Kutoka Aprili 1979 hadi Juni 2002 aliajiriwa na Shirika la Kilimo na Chakula (NAFCO). Mwezi Julai 2002 alijiunga na Chama cha wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania kama Afisa Mwandamizi wa Maendeleo wa TCCIA na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Kilimo. Yeye ni mjumbe wa Kamati ya Ukaguzi na Athari za Kampuni. Bi Mkocha ni mjumbe wa Bodi/Kamati zifuatazo:- Baraza la Kazi, Uchumi na Ustawi la Wizara ya Kazi, Bodi ya Nyama Tanzania, Kamati ya Taifa ya Usafi, Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya VETA na mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Ushauri ya Bodi ya Sukari Tanzania.
*Bi Mkocha ana uzoefu Zaidi ya miaka 10 kwenye Bodi. Na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).*

### BI MWANJAA SAID LYEZIA - MIAKA 45

Bi. Lyezia Ana Shahada ya Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya Uzamili ya Fedha kutoka Chuo kikuu cha Mzumbe. Ana uzoefu wa miaka 16 katika kazi. Ameajiriwa na Chuo Kikuu cha Mzumbe katika Nyanja tofauti kuanzia mwaka 2005 kama Mhasibu Msaidizi, Kampasi ya Dar es Salaam kuanzia mwaka 2005 hadi 2007, Mhasibu Mwandamizi mwaka 2008 hadi 2010 na kisha Mhasibu wa Kampasi ya Dar es Salaam mwaka 2011 hadi Aprili, 2018. Kuanzia April 2018 hadi 2019 aliteuliwa kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Fedha na baadaye kuteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Fedha, nafasi ambayo anaitumikia hadi sasa
*Bi Lyezia ana uzoefu Zaidi ya miaka 10 kwenye Bodi. Na pia amesajiliwa na Chuo cha Wakurugenzi Tanzania (IoDT).*

**JUMLA YA HISA ZILIZOLIPIWA: 73,077,253**

| CDS No. | JINA LA MWANAHISA | AINA YA UWAKILISHI | JINA LA MWAKILISHI | HISA | % HISA |
|---|---|---|---|---|---|
| 585373 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND | MWAKILISHI | HUGO MHINA | 28,100,300 | 38.4529 |
| 569364 | MKOMBOZI FISHING & MARING TRANSPORT LTD | MWAKILISHI | JOSEPH KAHUNGWA | 4,215,000 | 5.7679 |
| 569351 | ABBASI EXPORTS LTD | MWAKILISHI | A. SRINIVASA RAO | 1,686,000 | 2.3071 |
| 150344 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA | MWAKILISHI | JOSEPH KAHUNGWA | 1,405,000 | 1.9226 |
| 121481 | FAYAZ FEROZ RASHID | MWAKILISHI | ROSE OSIMA | 1,236,400 | 1.6919 |
| 46802 | NIMROD ELIREHEEMAH MKONO | MWAKILISHI | LEA MIDALA MKONO | 1,123,975 | 1.5381 |
| 105271 | LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA | BINAFSI | | 464,200 | 0.6352 |
| 55965 | ZAHIR WAZIRI LEYSUYAH | BINAFSI | | 210,737 | 0.2884 |
| 569202 | DR. STERGOMENA LAWRENCE TAX | BINAFSI | | 168,600 | 0.2307 |
| 100793 | ELISANTE ELIKANA MURO | BINAFSI | | 140,500 | 0.1923 |
| 124080 | MAGDALENA NELSON ENOCK MKOCHA | BINAFSI | | 102,362 | 0.1401 |
| 569106 | ASUNGWILE BASALILE MWANGUNGULU | BINAFSI | | 70,250 | 0.0961 |
| 514441 | MAGRETH JOHN MBILINYI | BINAFSI | | 56,200 | 0.0769 |
| 57608 | CHARLES JAMES MIHO | BINAFSI | | 56,200 | 0.0769 |
| 569576 | ABILAHI ALLY DARUSI | BINAFSI | | 56,200 | 0.0769 |
| 569326 | TCCIA DODOMA | BINAFSI | | 44,962 | 0.0615 |
| 569334 | TCCIA MTWARA | BINAFSI | | 28,100 | 0.0385 |
| 130704 | LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA | BINAFSI | | 23,380 | 0.0320 |
| 107592 | NATHAN EDWARD MNYAWAMI | BINAFSI | | 19,675 | 0.0269 |
| 569340 | TCCIA BARIADI BRANCH | BINAFSI | | 16,862 | 0.0231 |
| 569184 | JOEL TIMOTH CHIKOMA | BINAFSI | | 14,613 | 0.0200 |
| 228299 | ISARIA KAWEDI MWENDE | BINAFSI | | 12,500 | 0.0171 |
| 514523 | DONALD JIMOGI KAMORI | BINAFSI | | 12,500 | 0.0171 |
| 219736 | DONALD JIMOGI KAMORI | BINAFSI | | 11,238 | 0.0171 |
| 569825 | ARISTIDES JOHN NGOWI | BINAFSI | | 11,237 | 0.0154 |
| 515900 | JOAN JAMES MNGODO | MWAKILISHI | JIMMY S. MADATTA | 10,000 | 0.0137 |
| 569253 | ISMAIL SAI MKUMBWA | BINAFSI | | 5,625 | 0.0077 |
| 261544 | PETER ALBERT MASAWE | BINAFSI | | 5,000 | 0.0068 |
| 504917 | ISRAEL EMMANUEL KINGU | BINAFSI | | 5,000 | 0.0068 |
| 113206 | CHARLES JAMES MIHO | BINAFSI | | 5,000 | 0.0068 |
| 115405 | TUMAINI AKIRWA MUNISI | BINAFSI | | 5,000 | 0.0068 |
| 569197 | EDGAR JOEL KAHABWA | BINAFSI | | 4,413 | 0.0068 |
| 570372 | VENUS THOMAS SINDAMENYE | MWAKILISHI | AMAN VENACE | 4,212 | 0.0058 |
| 95037 | ISRAELEMMANUEL KINGU | BINAFSI | | 3,600 | 0.0049 |
| 569391 | BARTHOLOMEW MAJOR KUNZUGALA | BINAFSI | | 3,375 | 0.0046 |
| 569732 | AGNESS ROBERT LIMBU | BINAFSI | | 2,812 | 0.0038 |
| 570687 | SAMSON MAKOYE MALANDO | BINAFSI | | 2,812 | 0.0038 |
| | | BINAFSI | | 2,812 | 0.0038 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 569896 | THABITI JUMAA SHETUMBA | | | |
| 569836 | DEUSDEDIT TUNGI MANGWALA | BINAFSI | 1,400 | 0.0019 |
| 235269 | TUGURO ZAKAYO MBOTA | BINAFSI | 1,400 | 0.0019 |
| 569146 | DOMINIC DANIEL KYARUZI | BINAFSI | 1,400 | 0.0019 |
| 520040 | FRANK JULIUS MOLLEL | BINAFSI | 1,000 | 0.0014 |
| 546689 | LULU SILAS OLANG | BINAFSI | 1,000 | 0.0014 |
| 523022 | KELVIN ISAYA BIYA | BINAFSI | 500 | 0.0007 |
| 546276 | EMMANUEL EUSTACE ISHASI | BINAFSI | 400 | 0.0005 |
| 501156 | GODBLESS GIBSON MINJA | BINAFSI | 300 | 0.0004 |
| 585985 | PETER WILLIAM KIFUNGUOMALI | BINAFSI | 270 | 0.0004 |
| 510895 | PETER ANYANDWILE KAJUNI | BINAFSI | 250 | 0.0003 |
| 546905 | BERNARD MELEDITH ULAYA | BINAFSI | 200 | 0.0003 |
| 546908 | LEONIDAD RWEHUMBIZA KARUMUNA | BINAFSI | 100 | 0.0001 |
| 546909 | MICHAEL DEOGRATIUS MKANGI | BINAFSI | 100 | 0.0001 |
| 546275 | EMMANUEL E. ISHASI | BINAFSI | 100 | 0.0001 |
| 546446 | PETER JOHN LISUNGU | BINAFSI | 100 | 0.0001 |
| 546571 | KELVIN IVOD MATHIAS MOSHA | BINAFSI | 100 | 0.0001 |
| 121195 | EDGAR LUTAINULWA KAHABWA | BINAFSI | 70 | 0.0001 |
| 999999 | DIANA SALLANGA | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | KAMAL DAVADRA | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | GIDEON KAPANGE | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | NEEMA MONDOMA | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | ISHMAEL SAGIRAKI LAISSER | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | BENITHO KYANDO | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | MNARI | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | WITNESS GOWELLE | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | LILIAN NZUTI | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | DEOGRATIUS KAMAGI | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | JACQUELINE MALETHO | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | JAMES MAJUKANO | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | JOSEPHINE CHRISTOPHER | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | AZIZ MSUYA | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | DOMINIC DOMINIC | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | ERNEST KHISOMBI | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | IMTIAZ DATOO | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | KIBAMBI IBRAHIM | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| 999999 | EPHRAIM BAHEMU | WASIO WANAHISA | 0 | 0.0000 |
| **JUMLA** | | **75** | **39,745,784** | **54.3887** |

**TCCIA INVESTMENT PLC**
P.O.Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania
Tel: 255 – 22 – 276 0172/27601725
Fax: 255 – 22 – 2119437
Email: info@tcciainvest.co.tz,
Web site: http://www.tcciainvest.co.tz